**JINA: ______________________________________________ NAMBA YAKO ___________**

**SAHIHI ___________________________________TAREHE ___________________________**

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**LUGHA**
**JULAI/AGOSTI -2013**
**MUDA SAA 2 ½**

**JARIBIO LA MUUNGANO WA LAINAKU 2, 2013**
**KISWAHILI**
**KARATASI PILI**

**MAAGIZO**

1. Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
2. Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
3. Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.
4. Karatasi hii ina Kurasa **8** zilizopigwa chapa.
5. Watahiiwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |

| | | |
|---|---|---|
| **Jumla** | **80** | |

1. **UFAHAMU ( alama 15)**

**Soma makala yafutayo kisha ujibu maswali**

Maoni yetu juu ya uhuru tuliotwaa yanahitilafiana sana. Wao katika upande mmoja watu wanaofikiri kuwa kupewa uhuru ni kushikishwa upembo na kuambiwa: Haya jamaa oneni mitunda, pembeni mitunda mle mkasaze katika upande mwingine kuna wale wanaouona uhuru kama hali ya mtu kujihisi ana hiari na mamlaka ya juu ya jambo lolote lipasalo kutenda kwa mujibu wa maendeleo yake mwenyewe na ya jamaa kwa jumla. Kundi la tatu ni la wale wasiojua maana ya uhuru wao hukiri na kuitikia mara moja mawaidha wanayoshenezwa na viongozi wao.

Watu wa makundi haya matatu huwa hawana kosa kuwa katika hali waliyomo kwa kuwa hiyo ni hali ya kimaombile. Uhuru una maana ya kujitawala na kujitawala kuna maana ya kujihami,kujikimu,kujivalisha na kujiamlia.Endapo baa hiyo ndiyo maana ya uhuru hapana budi kundi la kwanza kujibu swali hili, "matunda wanayokawia kupeana yamepandwa na nani?". Karima alimhuluku mwanadamu na kuupangia mastakimu yake kisha akamjalia akili, uwezo na vitu vya kumpa chakula. Maumbile nayo yakatwaa, wadhifa wa kuyabadili mazingira alimoishi mwanadamu. Hapo ughali wa maisha ukadhihirika. Kwa hivyo ikamlazimu kutumia akili na nguvu kupambana na vita vya kimaumbile ili kudumisha uhai.

Wanachukua uhuru kuwa ni hali ya kujitegemea wana mawazo sadifu sana. Uhuru huweza kuelezwa katika sehemu mbili. Kwanza ni ile hali ya mtu kujikurupusha kutoka katika nyanyaso za mtu anayetawala kwa nguvu na kumtumikisha; ikiwa sasa hana ubwana juu yake.Pili, ni kule kupewa hatamu na kuachwa pekee

kumwendesha farasi usipomwendesha salama atakubwaga na kukuhasiri na mambo yatavurugika utakuwa umefuja. Tunao basi uhuru wa kimawazo na uhuru wa kiuchumi. Mawili haya hayaachani kama chungu na kia. Tukihisi kuwa tuko huru kimawazo tusiwe radhi na kuachia hapo. Hatuna budi pia kutazama upande wa uhuru wa kiuchumi.

Tulipoachiwa uamuzi wa mambo yetu wenyewe hakika tuliwekwa katika mizani kupimwa uwezo wetu wa kufanya kazi. Wajuzi wa mambo wamesema , "Uhuru ni kufanya kazi". Bila kufanya kazi kwa bidii uhuru hukosa maana. Uhuru una maana ya kujilimia mashamba, kustawisha ufugaji,kujijengea mashule, hospitali na vyumba vizuri vya kuishi, kujifundisha kuendelea kujitolea mhanga kazini na kuikuza jamii.

Kwa kuwa viongozi ni watu wanaotegemewa sana na wale wasiojua kujiendeleza. Yabainika wanalo jukumu kubwa na gumu kuwaleta watu hao katika mkururo wa watu wengine. Walio na mawazo ya kufanyiwa kazi huku wao wataanasa, itawapasa kujiuliza mara moja,mara mbili kama wana uhuru wa kweli?

**Maswali**

a) Ipe taarifa hili kichwa mwafaka (Alama 1)

..........................................................................................................................................

b) Eleza kwa muhtasari maana ya uhuru. (Alama 4)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

c) Kwa nini maana haieleweki kwa baadhi ya watu? (Alama 4)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

d) Sisi raia tulio huru tuna wajibu gani katika taarifa? (Alama 1)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

e) Fafanua wajibu wa viongozi katika taifa huru. (Alama 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

f) Eleza maana ya msamiati na vifungu vifuatavyo kama yalivyotumiwa katika taarifa.
i) Kushikishwa upembo ukapambe matunda (Alama 3)
..........................................................................................................................................

ii) Kula na kusaza.
..........................................................................................................................................

iii) Huku wao wataanasa.

..........................................................................................................................................

**2. MUHTASARI (Alama 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Maendeleo ni hali ya watu kuwa na uwezo wa kuishi maisha mazuri, kujithibiti na kujisimamia katika shughuli zao za kila siku. Hayati Mwalimu Nyerere alisema maendeleo ni kuwepo kwa hali inayowezesha watu kupunguza gharama za maisha. Kwa mfano, kuwepo kwa mfumo bora wa elimu, huduma bora za afya, usafiri na utawala bora ni baadhi ya mambo yanayoleta ufanisi katika maisha ya binadamu. Hivyo basi kuwepo kwa miradi, hali au vitu visivyosaidia binadamu si maendeleo. Aghalabu, vitu hivyo huwa vikwazo vinavyozuia maendeleo na kufanya maisha ya binadamu kuwa magumu.

Tangu asili na jadi, kikwazo kikubwa cha maendeleo kimekuwa itikadi za kijamii kisiasa na kiuchumi ambazo zinatenga kazi na mambo fulani, kuwa ya wanaume na mengine kuhusishwa na wanawake. Mathalani, miongoni mwa jamii nyingi za kiafrika wanawake wanaaminiwa kuwa viumbe duni. Inaaminiwa kuwa mwanamke ana upungufu wa kiakili na nguvu za mwili akilinganishwa na mwanaume. Kwa sababu ya dhana hii hafidhina na potovu, kuna kazi ambazo wanaume hawawezi kuzifanya eti kwa sababu ni za wanawake.

Katika sehemu za mashambani wanawake hufanya takribani kazi zote za nyumbani zikiwemo kuchana kuni, kupika, kulea watoto, kuuguza wagonjwa, kupokea wageni, kuosha na kulea watoto na kadhalika. Kazi hizi ni nyingi na humfunga mwanamke nyumbani. Kazi zilizotengewa wanaume ni chache na wao huwa na wakati mwingi wa kupumzika. Kwa mfano, ni nadra kumpata mwanaume wa kijijini akifanya kazi nyumbani

baada ya saa kumi za mchana. Nyakati kama hizi utawakuta wanaume kwenye vilabu vya pombe, mitaani wakitembea na hata kuzuru boma moja hadi nyingine. Utawakuta sokoni wameketi huku wameandika nne kwa miguu yao wakipiga gumzo. Ukiwauliza baadhi yao watasema ni masaa y kupumzika.

Jambo hili limekuwa kikwazo kikubwa cha maendeleo katika jamii kwa sababu wanaume hutumia wakati mwingi katika starehe badala ya kuzalisha mali.

Ardhi ndiyo rasilmali yenye dhamana kubwa kwani ndiyo inayomwezesha mtu kuzalisha mali. Hata hivyo, inasikitisha kuona kwamba wanawake wengi hasa wale wasioelimika hawana vyeti vya kumiliki ardhi. Hili ni tatizo kubwa kwa sababu panapotokea talaka kati ya mke na mume, mwanamke hurudi nyumbani kwa wazazi wake aghalabu bila kudai chochote.

Inasemekana kuwa mfumo mzuri wa siasa na uongozi katika jamii hufanikisha maisha mazuri. Vivyo hivyo, siasa mbaya ndicho kiini cha maisha mabaya. Katika mfumo wa siasa na uchumi idadi kubwa ya wanawake hubaguliwa na wanaume. Mwanamke anayezindua wenzake dhidi ya siasa mbaya na maonevu aghalabu husemekana amekiuka utamaduni na hataki kuthibitiwa na mwanaume. Jambo hili linawafanya wanawake kuchelea kujitokeza hadharani kupinga uongozi mbaya na maonevu.

Hata hivyo, kuna baadhi ya wanawake waliotia bidii maishani na kuthibitisha kwamba mwanamke ana uwezo sawa na mwanaume kwa mfano, nchini Kenya kuna wanawake waliojitokeza kifua mbele wakachaguliwa na hata kuteuliwa katika nyadhifa za uongozi. Wote hawa wana bidii za mchwa na wamestawisha maisha ya wananchi.

Katika nyanja za michezo, muziki, elimu na sheria, wanawake wamejizatiti na hata kuwashinda wanaume. Kwa mfano, katika michezo ya Olimpiki, timu za wanawake zimekuwa zikishinda nishani chungu nzima.

Katika elimu, tumeshuhudia wasichana wakiwashinda wavulana katika mitihani. Jambo hili limewawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika maswala tatizo kama vile udaktari na uanasheria. Mambo haya ni thibitisho kuwa tunapaswa kuwapa wanawake nafasi sawa na wanaume katika shughuli zote za jamii na ujenzi wa taifa. Ningehimiza wanaume wasiwe na inda na kinyongo dhidi ya wanawake kwani chanda chema huvishwa pete.

**MASWALI**

a) Kulingana na makala haya kuna vigezo vitatu vinavyoweza kutumiwa kuonyesha kiwango cha maendeleo katika jamii. Vionyeshe. (Maneno 20-25) (Alama 3)

Nakala Chafu

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………

Nakala Safi

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………--
------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

b) Kwa mujibu wa taarifa hii, kuna vikwazo gani vinavyozuia mwanamke kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo? (Alama 3)

Nakala Chafu

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

Nakala Safi

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

c) Dhana kwamba mwanamke ni kiumbe duni limepingwa na baadhi ya wanawake. Onyesha vipi. (Maneno 35-40)

(Alama 6)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

a) Onyesha shadda katika maneno yafuatayo . (alama 1)

i) Kuzungumza

…………………………………………………………………………………………………………

ii) Niletee

…………………………………………………………………………………………………………

b) Eleza matumizi mawili ya (ki) kisha utunge sentensi moja moja kuonyesha matumizi hayo.

(alama 4)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

c) Andika maana mbili za: (alama 2)

Tulimchezea Jumatatu

…………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

(d) Andika katika **usemi halisi**.

Kiptoo alimwambia shangazi yake kuwa angekuwa akienda kumtembelea kwake kila wiki. (alama3)

___

___

(e) Yakinisha katika **wingi**.

Hakukuarifu kuhusu yule hajala. (alama 2)

___

___

(f) Fafanua kwa kutungia sentensi **matumizi** mawili ya neno **namna**. (alama 2)

___

___

g) Tumia kirejeshi 'O' tamati katika sentesi hii.

Malipo ambayo anapewa ni yale ambayo yanaridhisha. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

h) Pambanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali.

Mwanafunzi hodari anayechezea shule ya Nangina amepewa zawadi. (alama 4)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

i) Taja vikwamizo viwili vinavyotamkiwa kwenye ufizi (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

j) Bainisha shamirisho kipozi, kitendo na ala katika sentensi hii. (alama 3)

Swalim alimletea Maria chai kwa chupa

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

k) Vielezi namna ni vya aina mbalimbali.

Tambua na ueleze vielezi vya namna vilivyotumika katika sentensi zifuatazo

i) Mtoto anapenda kulia ovyo ovyo jioni (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

ii) Juma alisafiri kwa ndege hadi Nairobi (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

l) Tunga sentensi ukitumia kitenzi <u>cha</u> katika hali ya kutendwa (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………

m) Bainisha vishazi katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Kisima ambacho kimejaa maji kitajengwa.

……………………………………………………………………………………………………

(n) (i) Unda nomino mbili kutokana na kitenzi 'ongopa' (alama 2)

(ii) **Tambulisha** aina za **nomino** katika sentensi ifuatayo. (alama 1)

Umma katika Jamhuri yetu unataka haki ya kila mja itekelezwe.

.

___________________________________________________________________________

(o) Vinyambue vitenzi vifuatavyo kulingana na maagizo. (alama 2)

(i) Ja ________________________________ (tendwa)

(ii) La ________________________________ (tendesha)

(iii) Nata ______________________________ (tendeshwa)

(iv) Juvya ______________________________ (tenda)

(p) Tunga sentensi yenye kihusishi cha 'a' – unganifu katika ngeli ya U – ZI. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

(q) Tofautisha: (alama 2)

i) Mwenye mali amefika.

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

ii) Mwenyewe anapendeza.

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

## 4. ISIMU JAMII (alama 10)

(a)Fafanua njia tofauti zilizotumiwa kueneza lugha ya Kiswahli nchini. (alama 5)

(b) Ni matatizo gani yaliyokumba maenezi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru? (alama 5)

**ANSWERS:**

Order a copy of answers from [www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy](www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy)

NB> We charge Kshs. 100 ONLY to meet website, e-resource compilation and provision costs